Kitabu cha Mwongozo na Ufahamu Juu ya

Sheria ya Kuzuia Na Kupambana Na Ukimwi ya 2008, Sheria Namba 28 ya 2008

Kimeandaliwa kwa Ushirika wa:-

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC); na
Shirika la Futures Group International kwa hisani ya mradi wa Public Health Initiative (PHI)

Kimetayarishwa na Kuharirіwa na: -

Theresia Kinabo, Clarence Kipobota na Rodrick Maro
wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)

Mchoraji ni: -
Xxxxxx Mmmmmmm

Visa Mafunzo Vimebuniwa na: -

Waandaaji wa Kitabu hiki kwa msaada wa machapisho mbalimbali na uzoefu wa LHRC katika kazi za jamii.

Wachapaji:

……

Toleo la Kwanza, Oktoba 2009
Dar es Salaam, Tanzania.

ISBN: 0000-000-00-0

© LHRC & FUTURES GROUP INTERNATIONAL
Oktoba, 2009

YALIYOMO

DIBAJI v
UTANGULIZI vi
Sehemu ya Kwanza 1
Maelezo na Ufafanuzi wa Awali 1
1.1 Jina na Kuanza Kutumika kwa Sheria 1
1.2 Madhumini ya Sheria Hii 1
Sehemu ya Pili 2
Majukumu ya Jumla 2
2.1 Majukumu ya Jumla 2
2.2 Wizara Kuendeleza Mikakati ya Usalama na Tahadhari 3
2.3 Majukumu Kisekta 3
Sehemu ya Tatu 5
Elimu ya Umma na Mipango Kuhusu VVU na UKIMWI 5
3.1 Elimu kwa Umma na Mipango Kuhusu VVU na UKIMWI 5
3.2 Usambazaji wa Taarifa juu ya VVU na UKIMWI 5
3.3 Elimu ya VVU na UKIMWI Mahala pa Kazi 5
3.4 Mafunzo kwa Wataalamu wa Afya 5
3.5 Uchangiaji wa Tishu, Viungo, Damu na Mazao ya Damu 6
3.6 Upasuaji, Matibabu ya Meno na Taratibu kama hizo 6
Sehemu ya Nne 8
Ushauri na Kupima 8
4.1 Kupima VVU 8
4.2 Ushauri 8
4.3 Kuzuia Upimaji wa VVU kwa Lazima 8
4.4 Majibu ya Upimaji 10
Sehemu ya Tano 11
Usiri 11
5.1 Usiri wa Kitabibu 11
5.2 Mambo yanayoweza Kutokuzingatia Usiri wa Kitabibu 11
Sehemu ya Sita 12
Afya na Huduma Muhimu 12
6.1 Huduma za Msingi za Afya kwa Watu wenye VVU na UKIMWI 12
6.2 Mipango ya Kujikimu, Stadi za Kimaisha na Kupunguza Makali ya UKIMWI 12
6.3 Kuzuia Maambukizi kwa Kumjulisha Mwenza na Kuchukua Tahadhari 13
6.4 Kuzuia na Kupambana na Magonjwa ya Zinaa 14
6.5 Matumizi ya Kondomu 14
6.6 Kufikiwa kwa Huduma za Afya 14
6.7 Kuzuia Maambukizi kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto 15
6.8 Kuambukizwa Ugonjwa wa UKIMWI wakati wa Matibabu 16
6.9 Taarifa Potofu 16
Sehemu ya Saba 17
Unyanyapaa na Ubaguzi 17
7.1 Kuzuia utungwaji wa Sheria, Sera na Taratibu za Kiubaguzi 17
7.2 Kukatazwa kwa Wahudumu wa Afya Kunyanyapaa 17
7.3 Kukatazwa kwa Aina nyinginezo za Unyanyapaa na Ubaguzi 17

7.4 Makosa yatokanayo na Unyanyapaa na Ubaguzi 18
Sehemu ya Nane 19
Haki na Wajibu wa Watu Wanaoishi na VVU na UKIMWI 19
8.1 Haki na Wajibu wa watu wenye VVU na UKIMWI, Yatima na Wengine 19
8.2 Upatikanaji wa Huduma Muhimu za Elimu na Afya 19
8.3 Kukatazwa kwa Matumizi mabaya ya Misaada kwa AZISE na Taasisi za Kiserikali 20
Sehemu ya Tisa 22
Kuanzishwa Kwa Kamati ya Utafiti 22
9.1 Kamati ya Taifa ya Wanazuoni wa Utafiti wa VVU na UKIMWI 22
9.2 Majukumu ya Kamati 22
9.3 Maadili ya Kitaaluma 23
Sehemu ya Kumi 24
Ufuatiliaji wa Tathmini 24
10.1 Ufuatiliaji 24
10.2 Utoaji wa Taarifa kwa Huduma za Afya 24
10.3 Uchunguzi wa Magonjwa na Utoaji wa Taarifa 24
Sehemu ya Kumi na Moja 25
Makosa na Adhabu 25
11.1 Makosa yanayotokana na Kukiuka Haki ya Usiri 25
11.2 Makosa yanayotokana na kuambukiza/Kuenea kwa VVU 25
11.3 Makosa yanayotokana na kukiuka Taratibu za Kiusalama kunakosababisha Kuenea kwa VVU 26
11.4 Adhabu kwa Makosa yatokanayo na Kuzuia Utekelezaji wa Sheria Hii 26
11.5 Adhabu za Jumla 27
Sehemu ya Kumi na Mbili 28
Vifungu Anuwai (Mchanganyiko) 28
12.1 Malalamiko 28
12.2 Kanuni 28
12.3 Zuio/katazo la kulazimisha (lazimisho) 29
MUHTASARI WA SHERIA YA UKIMWI 30

DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kwa kushirikiana na Shirika la Futures Group International kupita mradi wa Health Policy Initiative (HPI) tumeona ni vyema kuandaa tafsiri hii rahisi ya sheria ya kuzuia na kupambana na VVU na UKIMWI. Kitabu hiki kimeandaliwa kwa kumefuata maelekezo kama ilivyo katika *Sheria ya Kuzuia na Kupambana na VVU na UKIMWI ya 2008, Sheria Namba 28 ya mwaka 2008*.

Umuhimu wa kuandaa kijitabu hiki ni kutaka kuifafanua vyema Sheria hiyo katika lugha nyepesi ili iweze kuwafikia watu wengi, kwani sheria nyingi huandaliwa kwa lugha ya kitaalamu na mara nyingine ya kigeni, hivyo kuzuia kueleweka kirahisi na kufanya makosa kuendelea kujitokeza. Pia, matumizi ya vielelezo (katuni na visa mafunzo) yatamsaidia msomaji kufafanua zaidi mambo yaliyotajwa katika kitabu hiki.

Katika mapambano dhidi ya kuenea kwa VVU na UKIMWI, taarifa za kweli na sahihi ni muhimu sana. Matumizi ya sheria ni moja ya mikakati muhimu sana katika vita dhidi ya VVU na UKIMWI. Tunaunga mkono juhudi zozote zinazofanywa na serikali pamoja na wadau wengine katika kukabiliana na janga hili la VVU na UKIMWI ili kujenga jamii na taifa lenye afya na nguvu ili kukuza ustawi wake.

Ni mategemeo yetu kuwa tafsiri hii rahisi ya *Sheria ya Kuzuia na Kupambana na VVU na UKIMWI ya 2008* itawasaidia walio wengi kuelewa haki na wajibu walionao na hivyo kusaidia walio wengi kuelewa haki na wajibu walionao na hivyo kusaidia juhudi za serikali na dunia nzima katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Maelezo mengi ya sheria hii yanategemeana, hivyo ni vyema kukisoma kitabu hiki kwa ujumla wake ili kuweza kuelewa kwa undani masharti na maelekezo ya sheria hii.

Tunatoa wito kwa serikali, mashirika ya kijamii na wadau mbalimbali kuweza kuendeleza mapambano haya. Hatua za ziada na za makusudi zichukuliwe ili kulinda haki za binadamu za watu wenye VVU na UKIMWI. Elimu ya afya kwa umma hususan juu ya VVU na UKIMWI lazima ipewe kipaumbele ili kulinda afya na kutetea haki za binadamu. Taarifa muhimu na sahihi juu ya VVU na UKIMWI itolewe kwa nguvu zote katika kila kona ya nchi ili kupunguza maambukizi ya VVU na kuongeza huduma bora na kuwajali walioathirika na wanaoishi na VVU na UKIMWI.

Vita dhidi ya UKIMWI na VVU inawezekana, jua haki zako, timiza wajibu wako.

UTANGULIZI

Sheria ya Kuzuia na Kupambana na VVU na UKIMWI ya Mwaka 2008, imetungwa kwa lengo la kutekeleza Sera ya Taifa ya Kudhibiti VVU na UKIMWI ya mwaka 2001. Sheria hii ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Mungano wa Tanzania mwaka 2008. Tarehe 4 Aprili, 2008, Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, aliweka saini ili kuidhinisha kuanza kutumika rasmi kwa sheria hii.

Sheria hii inalenga katika kusimamia masuala ya kinga, huduma na kuzuia kuenea kwa VVU na UKIMWI; kusimamia huduma za afya kwa umma hususan zile zinazoshabihiana na VVU na UKIMWI. Pia inahusika katika usimamiaji wa utoaji tiba sahihi, huduma na uangalizi kwa kutumia rasilimali zilizopo kwa watu waishio na/ama walio katika hatari ya kuambukizwa VVU na UKIMWI na kusimamia utoaji huduma zinazoendana nazo.

Vilevile, sheria hii inatoa mwongozo wa jinsi ya kupambana na janga la VVU na UKIMWI, ikibainisha ukubwa wa janga hilo na maelekezo juu ya haki na wajibu wa watu waishio na VVU na UKIMWI. Pia sheria hii inaunganisha nguvu za sekta mbalimbali zilizo katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kisheria na kimaadili na kulinda haki za walioathirika na VVU na UKIMWI na familia zao. Masuala ya tafiti za kisayansi na wajibu wa watafiti yameainishwa katika sheria hii kwa undani pia.

Kwa upande wa usimamiaji wa masharti mengi yaliyomo katika sheria hii, vifungu mbalimbali vya sheria vinaonyesha kuwa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya Tanzania (TACAIDS) kuwa ndiyo itakuwa na jukumu la awali la kusimamia masuala yote ya UKIMWI. Kuna taasisi nyingine pia zimetajwa kama wasimamizi wa vifungu vya sheria hii. Hata hivyo, kwa sehemu kubwa, jukumu la kinga na mapambano dhidi ya UKIMWI limeelekezwa kwa taasisi na watu wote.

Ukiukwaji wa masharti ya sheria hii ni kosa la jinai na pia mwathirika anaweza kufungua keshi ya madai. Utaratibu wa kufuatilia ukiukwaji wa haki na wajibu kama vilivyoainishwa katika sheria hii pia umeelekezwa.

Sheria hii inasomeka pamoja na sheria nyingine nyingi tu ambazo zinaanzisha taasisi mbali mbali, za mienendo wa makosa ya jinai na daawa pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu.

Sheria ya Kuzuia na Kupambana na UKIMWI ya 2008 ilianza kutumika mwaka 2008. Kutungwa kwa sheria hii, kunaifanya Tanzania kuwa moja kati ya nchi chache sana duniani ambazo zina sheria mahusisi kwa ajili ya kusimamia masuala ya VVU, UKIMWI na mambo yatokanayo na hayo.

Sheria hii inalenga hasa katika kutatua changamoto zitokanazo na masuala ya UKIMWI ikiwa ni pamoja na matunzo ya watoto yatima, haki na wajibu kwa watu waishio na VVU na UKIMWI pamoja na majukumu ya taasisi na watu mbalimbali.

Sheria hii imejaribu kwa sehemu kubwa kukataza mambo ambayo yamesababisha kuenea kwa UKIMWI ikiwa ni pamoja na tabia ya baadhi ya watu kuambukiza watu wengine VVU na UKIMWI kwa makusudi.

Sheria hii hailengi katika kukinzana na sheria nyingine zilizopo, ila ina lengo la kuchangia jitihada za sheria nyingine katika kusimamia masuala muhimu ya Jamii ya watanzania.

Sehemu ya Kwanza

Maelezo na Ufafanuzi wa Awali

1.1 Jina na Kuanza Kutumika kwa Sheria

Sheria ya Kuzuia na Kupambana na VVU na UKIMWI ya Mwaka 2008, imetungwa kwa lengo la kutekeleza Sera ya Taifa ya Kudhibiti VVU na UKIMWI ya mwaka 2001. Sheria hii ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Mungano wa Tanzania mwaka 2008. Tarehe 4 Aprili, 2008, Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, aliweka saini ili kuidhinisha kuanza kutumika kwa sheria hii.

1.2 Madhumini ya Sheria Hii

Sheria hii inalenga katika kusimamia masuala ya kinga, huduma na kuzuia kuenea kwa VVU na UKIMWI; kusimamia huduma za afya kwa umma hususani zinazoshabihiana na VVU na UKIMWI. Pia inahusika katika usimamiaji wa utoaji tiba sahihi, huduma na uangalizi kwa kutumia rasilimali zilizopo kwa watu waishio na ama walio katika hatari ya kuambukizwa VVU na UKIMWI na kusimamia utoaji huduma zinazoendana nazo.

Vilevile, sheria hii inatoa mwongozo wa jinsi ya kupambana na janga la VVU na UKIMWI, ikibainisha ukubwa wa janga hilo na maelekezo juu ya haki na wajibu wa watu waishio na VVU na UKIMWI. Pia sheria hii inaunganisha nguvu za sekta mbalimbali zilizo katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kisheria na kimaadili na kulinda haki za walioathirika na VVU na UKIMWI na familia zao. Masuala ya tafiti a kisayansi na wajibu wa watafiti yameainishwa katika sheria hii kwa undani pia.

Kwa upande wa usimamiaji wa masharti mengi yaliyomo katika sheria hii, vifungu mbalimbali vya sheria vinaonyesha kuwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI ya Tanzania (TACAIDS) kuwa ndiyo itakuwa na jukumu la awali la kusimamia masuala yote ya UKIMWI. Kuna taasisi nyingine pia zimetajwa kama wasimamizi wa vifungu vya sheria hii. Hata hivyo, kwa sehemu kubwa, jukumu la kinga na mapambano dhidi ya UKIMWI limeelekezwa kwa taasisi na watu wote.

Ukiukwaji wa masharti ya sheria hii ni kosa la jinai na pia muhanga anaweza kufungua keshi ya madai. Utaratibu wa kufuatilia ukiukwaji wa haki na wajibu kama vilivyoainishwa katika sheria hii pia umeelekezwa.

Sheria hii inasomeka pamoja na sheria nyingine nyingi tu ambazo zinaanzisha taasisi mbali mbali, za mienendo wa makosa ya jinai na daawa pamoja na Katiba ya Tanzania na Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu.

Sehemu ya Pili

Majukumu ya Jumla

2.1 Majukumu ya Jumla

Kifungu cha 4 cha Sheria kimeainisha watu wote, taasisi na mashirika yaliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania kuhakikisha kuwa wanafanya mambo yafuatayo: -

(a) Kusimamia na kutoa uelewa wa kutosha kuhusu chanzo na maambukizi, njia za maambukizi, madhara ya kuambikizwa VVU na UKIMWI na hata kinga na udhibiti wa maambukizo.

(b) Kupunguza maambukizi ya UKIMWI na VVU pamoja na kueneza magonjwa ya zinaa pamoja na kupunguza madhara yatokanayo na maambukizi ya UKIMWI na VVU kwa watu walio chini ya usimamizi wake.

(c) Kulinda haki za watoto yatima kwa kuwapatia afya bora pamoja na mahitaji muhimu ya kijamii, kuepuka kulazimisha upimaji wa UKIMWI na VVU isipokuwa kama sheria hii itasema hivyo na kupinga unyanyapaa na ubaguzi.

(d) Kupiga vita mawazo potofu juu ya mila na desturi mbaya zinazoweza kusidisha kuenea kwa UKIMWI na VVU katika jamii.

(e) Kutangaza mila na desturi zote potofu zinazoweza kusaidia kupunguza kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI na VVU kwenye jamii.

(f) Kuimarisha njia za upatikanaji wa matunzo na misaada mbalimbali kwa watu wanaoishi na VVU kutoka kwenye vituo vya afya na wanajamii.

Pia kifungu hicho cha Sheria hii, kimetoa wajibu kwa serikali, wanasiasa, viongozi wa dini, waganga wa jadi na waajiri kwenye sekta binafsi kufanya mambo yafuatayo: -

(a) Kutoa kipaumbele katika shughuli zote zinazohusiana na VVU na UKIMWI pamoja na kuonyesha taswira chanya kwa umma kuhusu UKIMWI na VVU.

> **ANGALIZO:** Kwa kutambua kuwa UKIMWI ni Janga la Kitaifa, na kuwa linamomonyoa nguvu kazi kwa maendeleo ya jamii na hivyo kufanya tushindwe kufikia Malengo ya Milenia ya Umoja wa Mataifa, Serikali ya Tanzania iliweka kampeni dhidi ya UKIMWI kama ni moja ya malengo yake katika Mkakati wa Kitaifa wa Kuondoa Umasikini na Kukuza Uchumi (MKUKUTA). [Tazama Aya 2.4.4 ya MKUKUTA, June 2005 na Aya 1.1 ya Sera ya Taifa ya UKIMWI ya 2001],

(b) Kutetea na kupinga unyanyapa na ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na VVU na UKIMWI.

Kwa mujibu wa sheria hii, watu wote, taasisi, mashirika, serikali, wanasiasa, viongozi wa dini, waganga wa jadi na waajiri katika sekta binafsi kushirikiana na **Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS)** ili kuhakikisha kuwa rasilimali zinagawanywa sawasawa nchini kote kwa lengo la kuepusha mrundikano wa rasilimali kwenye maeneo machache tu ya nchi.

> **ANGALIZO:** Tume ya Taifa ya Kuthibiti Ukimwi (TACAIDS) iliundwa mwaka 2001 na ***Sheria ya Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2001 (Sura ya 379 ya Sheria za***

Tanzania) ili kuratibu shughuli za UKIMWI kitaifa na baadaye kuundwa kwa kamati za pamoja za UKIMWI kuanzia ngazi za wilaya mpaka vijiji. Kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha sheria ya TACAIDS, Tume hii inaratibu shughuli zake kwa njia ya sera, miongozo inayoitoa na kadhalika. Hata hivyo, inaratibu shughuli hizo kwa upande wa Tanzania Bara peke yake. Kwa upande wa Zanzibar, kuna Tume nyingine kama hii.

Kumekuwepo na vipingamizi kadhaa katika kutekeleza kazi za kupambana na UKIMWI ambavyo vinatokana na mgawanyo wa bajeti na uratibu wa shughuli zake. Baadhi ya vikwazo hivyo ni: -

(a) Kamati za usimamizi wa pamoja za UKIMWI katika ngazi ya wilaya, kata na vijiji ziliundwa kwa usimamizi wa kitengo cha Maendeleo ya jamii katika wilaya lakini hawakutengewa bajeti.

(b) Asasi zisizo za serikali (AZISE), mashirika ya dini, watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, vijana na wanawake walichukuliwa kama washirika wadogo/wasio rasmi jambo ambalo limesababisha kutokuwa na usawa kati ya serikali na AZISE kwenye mgawanyo wa bajeti za UKIMWI.

(c) Mratibu wa shughuli za UKIMWI katika Halmashauri anawajibika kuratibu shughuli za UKIMWI katika wilaya yake lakini yeye mwenyewe siyo mjumbe wa Kamati ya Afya ya Wilaya ambayo inasimamia sehemu kubwa ya fedha za UKIMWI.

Hata hivyo, sehemu kubwa ya changamoto hizi zinatolewa majibu kwa kiasi fulani katika *Sheria ya Kuzuia na Kupambana na UKIMWI ya 2008* kama ambavyo imeonyeshwa katika kitabu hiki. Mambo mengine ya kifedha yanatakiwa kusimamiwa kwa mujibu wa Sheria nyingize, mfano Sheria za Serikali za Mitaa kwa sababu, Sheria ya UKIMWI haikatazi utumikaji wa sheria nyingine katika usimamizi wa masuala hata yanayohusu UKIMWI.

2.2 Wizara Kuendeleza Mikakati ya Usalama na Tahadhari

Sheria imetoa wajibu kwa Wizara ya Afya kuimarisha usalama wa afya na kutoa tahadhari dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI. Kwa mujibu wa Kifungu cha 5, Wizara imepewa jukumu ka kuimarisha usalama wa afya kwa kiwango cha juu na kutoa tahadhari ya ulimwengu juu ya kupiga vita taratibu zisizo za kitaalamu ili kupunguza hatari ya maambukizi ya VVU na UKIMWI.

Sheria inasema kuwa, Wizara inapaswa kutoa usalama (uangalizi) na tahadhari za ujumla katika madawa na taratibu za kimatibabu ili kupunguza uwezekano wa maambukizi ya VVU na UKIMWI.

2.3 Majukumu Kisekta

Kifungu cha 6 kinatoa majukumu ya kisekta kwa asasi mbalimbali kwa kuagiza pia zizingatie masuala la jinsia na ulemavu. Kifungu hicho kinasema kuwa, taasisi za serikali

na zile za binafsi, wakala, serikali za mitaa na mashirika mbalimbali lazima ziandae na kutekeleza mipango ya kupambana na VVU na UKIMWI inayohusisha jinsia na walemavu. Pia kwa kushirikiana na serikali, taasisi hizi zinapaswa kuwa na mipango endelevu katika kuzuia, kutoa huduma na kupambana na maambukizi ya VVU na UKIMWI. Baada ya kuandaliwa mipango hii yote lazima iwasilishwe kwa TACAIDS.kwa ajili ya uratibu kama sheria ya TACAIDS inavyoelekeza.

Sehemu ya Tatu

Elimu ya Umma na Mipango Kuhusu VVU na UKIMWI

3.1 Elimu kwa Umma na Mipango Kuhusu VVU na UKIMWI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 7, ni jukumu la Wizara ya Afya kushauriana na serikali za mitaa na wadau wengine ili kuandaa programu ya elimu yenge lengo la kuzuia ubaguzi na unyanyapaa dhidi ya wanaoishi na VVU na UKIMWI wanaoudumiwa. Wadua kwa maana ya sheria hii ni pamoja na vijana ambao kwa sehemu kubwa ndiyo waathirika wakubwa wa UKIMWI.

3.2 Usambazaji wa Taarifa juu ya VVU na UKIMWI

Sheria inaagiza usambazaji wa taarifa sahihi kuhusu VVU na UKIMWI. Kifungu cha 8 cha sheria kinasema kuwa, Wizara ya Afya, wataalamu wa afya, wafanyakazi katika taasisi za serikali na binafsi pamoja na Asasi za Kiraia zinapaswa kuhakikisha usambazaji wa taarifa kwa umma kama sehemu ya elimu ya VVU na UKIMWI. Pia, elimu hii ya VVU na UKIMWI inapaswa kuwa sehemu ya utoaji wa huduma za afya ambapo wadau wote wanohusika wanapaswa kuitoa katika njia muafaka, kwa kutumia teknolojia stahiki na inayoweza kufikiwa na watu wenye ulemavu.

Insert an illustration

3.3 Elimu ya VVU na UKIMWI Mahala pa Kazi

Sheria pia imetilia umuhimu suala la mapambano dhidi ya UKIMWI sehemu za kazi. Kifungu cha 9 cha sheria hii kinasema kuwa, waajiri wote kwa kushirikiana na wizara wanawajibika kuandaa na kuratibu programu za VVU na UKIMWI mahala pa kazi kwa wafanyakazi wake ambapo zitajumuisha elimu ya jinsia juu ya VVU na UKIMWI, usambazaji wa kondomu na matunzo kwa watu wanaishi na VVU na UKIMWI.

3.4 Mafunzo kwa Wataalamu wa Afya

Ili kuhakikisha kuzuia na kudhibiti maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa umma, kwa mujibu wa kifungu cha 10, Wizara inatakiwa kuandaa na kutekeleza programu za kuwafundisha wataalamu wa afya juu ya mbinu za tahadhari dhidi ya VVU/UKIMWI na magonjwa ya zinaa na taratibu za matibabu ambapo programu hizo zitatekelezwa na taasisi za afya pale rasilimali zitakaporuhusu.

3.5 Uchangiaji wa Tishu, Viungo, Damu na Mazao ya Damu

Sheria inaelekeza kuwa, mtu yoyote anaweza kwa hiari yake kuchangia tishu, viungo, damu ama mazao ya damu katika maabara na taasisi rasmi/zinazotambulika ambapo taasisi ama maabara hizo zitakubali mchango huo ikiwa tu vitu hivyo vitagundulika kutokuwa na VVU.
Pia kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha sheria hii, Maabara ama taasisi hizo hazipaswi kutumia mchango huo kama utangundulika kuwa na VVU. Mchango wowote ule utakaogundulika kuwa na VVU unapaswa kutupwa mara moja na kwa uangalifu mkubwa.

Mtu awaye yote atakayekwenda kinyume na vifungu hivi anafanya kosa na anapaswa kuadhibiwa: -

(a) Kama ni mtu binafsi atapigwa faini isiyo chini ya shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja ama kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au;
(b) Kama ni maabara au taasisi itapigwa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi milioni kumi.

3.6 Upasuaji, Matibabu ya Meno na Taratibu kama hizo

Kuhusu masuala yanayotokana na upasuaji na aina nyingine za utabibu kama hizo, Kifungu cha 12 kimeweka masharti kadhaa ya kiusalama. Kifungu hicho kinasema kuwa, wakati wa utoaji huduma za upasuaji, huduma za kinywa na meno na kazi/huduma nyingine zinazofanana na hizo, Sheria inawataka wataalamu wa afya kuzingatia yafuatayo: -

(a) Vifaa vyenye ncha kali vinapaswa kutumiwa kwa uangalifu wa hali ya juu.
(b) Wakati wa utoaji wa huduma za afya na hususan wakati wa kuwahudumia majeruhi wa ajali, tahadhari muhimu ni lazima zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kuvaa glavu, miwani ya kujikinga na mavazi maalumu.
(c) Kushika kwa tahadhari kubwa sindano na vifaa vingine vya kupimia damu.
(d) Kushika kwa tahadhari kubwa na kutupa/kutunza vyema maji maji yote ya mwili ama uchafu wa mtu anayefahamika kuwa na ama kuaminika kuishi na VVU.

Sehemu ya kifungu hicho kinawaagiza wamiliki, wasimamizi au mameneja wa huduma za afya kuwajibika na kuhakikisha yafuatayo: -

(a) Kuhakikisha huduma za madawa ya kujikinga kwa wahudumu wa afya, hususan baada ya kutoa huduma.
(b) Kutoa nyenzo na vifaa muhimu vya kufanyia kazi kama vile glavu, miwani ya kujikinga na mavazi maalumu.

(c) Kuhakikisha utunzaji mzuri wa sindano zilizotumika, vifaa vilivyotumika kupimi adamu, maji maji yoyote ya mwilini na uchafu mwingine kutoka kwa mtu mwenye VVU au anayedhaniwa kuwa na VVU.

Yeyote atakayekwenda kinyume cha vifungu hivi atakuwa amefanya kosa na ikithibitika atapaswa kulipa faini isiyopungua shilini laki tano.

[Insert Mchoro wa kutunza au kuangamiza vifaa vilivyotumika kupima VVU]

Sehemu ya Nne

Ushauri na Kupima

4.1 Kupima VVU

Vituo vyote vya huduma za afya vya umma na vituo vya ushauri na upimaji vinavyotambuliwa na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, vimepewa hadhi ya kuwa vituo vya upimaji ili kukidhi matakwa ya sheria hii. Pia Bodi ya Maabara za Afya za Binafsi, zinaweza kufanya hivyo endapo zitaruhusiwa na serikali kwa kuchapisha majina yao na kuvitangaza katika gazeti la serikali kuwa vituo cha upimaji.

Kuhusu watendaji, Kifungu cha 13 kinaelekeza kuwa, kila mtaalamu wa afya, anayefanya ama anayejihusisha na upimaji wa VVU anapaswa kuchukua tahadhari ili kuhakikisha yafuatayo yanafanyika: -

(a) Mchakato wa upimaji unafanyika mara moja na kwa umakini sana;
(b) Majibu ya vipimo vya VVU yanawasilishwa kama sheria hii inavyoagiza.

Hivyo basi, kwa mujibu wa sheria hii, mtu anapaswa kufanyiwa vipimo vya VVU katika vituo vilivyoainishwa katika kifungu hiki cha 13 pekee na si vinginevyo.

4.2 Ushauri

Kifungu cha 14 kinaagiza kuzingatia utoaji ushauri wakati wa mchakato wa upimaji VVU. Pia, kifungu hiki kimeweka maagizo ya kizingatia ufikiaji huduma hata kwa watu wenye ulemavu. Kifungu hicho kinaagiza kuwa, mmiliki yeyote, meneja ama msimamizi wa kituo cha upimaji anapaswa kuhakikisha kuwa kituo kinafikika na watu wenye ulemavu, na pia kunakuwa na mtaalamu wa kutoa ushauri kabla na baada ya kupima kwa mtu anayopimwa na pale inapobidi kwa mtu mwingine anayeweza kuathirika na matokeo hayo.

[Insert Case Cartoon]

4.3 Kuzuia Upimaji wa VVU kwa Lazima

Mtu yeyote aishiye Tanzania ana hiari ya kupima afya yake kwa kupima VVU bila kulazimishwa. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kifungu cha 15, mtoto ama mtu asiyeweza kupokea majibu ya vipimo vya VVU kama vile mlemavu wa akili, mtu mzee sana asiyejitabua, mtu mgonjwa sana asiyejiweza kiakili na wengine wenye shida kama hizo, anaweza kupimwa kwa ridhaa ya maandishi ya wazazi ama walezi. Hakuna mtu atakayelazimishwa kupima VVU.

Hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali, muhusika anaweza kupimwa hata pasipo hiari yake kama ilivyosemwa hapo juu. Sheria hii inasema kuwa, mtu anaweza kupimwa VVU pasipo hata ridhaa yake endapo: -

(a) Kama ni kwa amri ya Mahakama kwamba mtu huyo apimwe kwa ajili ya mchakato wa kesi inayomuhusu;
(b) Kama ni mchangiaji wa viungo vya binadamu na tishu, na;
(c) Kwa wenye makosa ya kujamiiana.

Kisa Mkasa: Ushauri, kupima na majibu: Vifungu vya 14, 15, 16

Baada ya kupata barua ya kuitwa kwenye usaili, Amani alifurahi sana. Siku hiyo ya usaili kulikuwa na watu toka tasasisi ya UKIMWI na waliletwa kwa ajili ya kuwapima watu wote watakaofaulu usaili kabla hawajapewa mikataba ya ajira. Kwa kuwa hakuwa na njia mbadala ya kupata kazi nyingine, Amani alilazimika kupimwa kwa sababu ndiyo sharti la kupata kazi.

Wakati wa kupima, mtaalamu bila kumwambia chochote alimwambia anyooshe mkono akatoa damu ya Amani. Kisha akamwambia "*nenda nimemaliza*".

Baada ya takribani dakika 25 yule mtaalamu alimpita Amani akiwa amebeba makaratasi na kwenda nayo kwa Mkuu wa Kampuni iliyomfanyia usaili wa kazi bwana Amani. Baada ya muda bwana Amani alitaarifiwa na Mkuu huyo kuwa *"umeshindwa kukidhi masharti kwa sababu wewe ni mgonjwa wa kudumu"*. Amani aliweweseka sana, *"ila ndiyo hivyo tena, Mungu hajapenda"*, alisema Amani huku akiondoka eneo la usaili.

Je ni kosa gani lililofanyika hapa? Ungekuwa kwenye nafasi ya Amani ungechukua hatua gani?

Kuhusu wanawake wajawazito, sheria inaelekeza kuwa, kila mwanamke mjamzito na mwanaume anayehusika na ujauzito huo au mwenza wa ndoa na mtu mwingine yeyote anayehudhuria huduma za afya, atashauriwa na kupewa huduma ya kupima VVU kwa hiari. Wataalamu wote wa afya, waganga wa jadi na wataalamu wa tiba za asili, wakunga wa jadi na wale wote wanohudumia wagonjwa wanatakiwa kuhimizwa kupima.

Mtaalamu yeyote wa afya atakayemlazimisha mtu yeyote kupima VVU au kumsababisha mtu mwingine kupima bila kuelewa kinachoendelea, atakuwa amefanya kosa.

Hata hivyo, bila kuathiri vifungu vya sheria hii vilivyotangulia, mtaalamu wa afya mwenye jukumu la kuhakikisha matibabu ya mtu mwingine, anaweza kumpima VVU bila ridhaa yake iwapo tu kama: -

(a) Mtu huyo hajitambui na hivyo kushindwa kuridhia;
(b) Kama mtaalamu huyo anaamini kuwa ni muhimu sana ama pengne ni lazima kumpima mtu huyo kwa manufaa binafsi ya mtu huyo.

Kisa Mkasa - Kupima kwa Hiari: Kifungu cha 15

Emmanuel ambaye ni mwanamziki mashuhuri alikuwa kipenzi cha akina dada. Baada ya mwaka, hali yake ilianza kudhoofika. Muuguzi alimshauri apime UKIMWI. Emmanel akakataa. Taarifa zilipomfikia mganga mkuu, ambaye ni mjomba wake Emmanuel aliamuru nesi amchukue vipimo vya siri halafu wampime UKIMWI. Mbinu hii ilifanikiwa ila maabara hawakutoa majibu kwa mganga mkuu isipokuwa shabiki mkuu wa mfadhili wa Emmanuel tayari keshamwambia majibu ya "kijana wake".

Ni haki gani aliyokiukiwa Emmanuel?
Je, Mganga mkuu wa hospitali alitenda kosa lolote kisheria?

4.4 Majibu ya Upimaji

Sera na Sheria za UKIMWI vinakataza utoaji wa majibu pasipo ridhaa ya muhusika ama mlezi wake. Usiri no moja ya Haki za msingi za binadamu kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania na Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu.

Kifungu cha 16 cha Sheria hii ya UKIMWI inasema kuwa, majibu ya matokeo ya vipimo vya VVU yatakuwa ni siri na yanapaswa kutolewa tu kwa mtu aliyepimwa. Hata hivyo, bila kuathiri kifungu hiki, majibu hayo yanaweza kutolewa kwa watu wafuatao: -

(a) Wazazi au walezi iwapo aliyepimwa ni mtoto;
(b) Mwenza ama mlezi iwapo aliyepkimwa atakuwa katika hali ya kutoweza kuyapokea;
(c) Mwenza au mshiriki kingono wa mtu aliyepima;
(d) Mahakama, iwapo italazimika kufanya hivyo.

Sehemu ya Tano

Usiri

5.1 Usiri wa Kitabibu

Kifungu cha 17 cha sheria ya UKIMWI kinaagiza kuwa, wataalamu wote wa afya, wafanyakazi, waajiri, makampuni ya ajira, makampuni ya bima, wataalamu wa takwimu, wafasiri wa lugha ya alama, walezi kisheria na waangalizi wote wa kumbukumbu za kitabibu, nyaraka na takwimu au majibu ya vipimo ni lazima watunze usiri wakati wakishughulika na taarifa za kitabibu na nyaraka mbalimbali, hususan utamblisho na hali ya mtu anayeishi na VVU na UKIMWI. Kwa mtu yeyote aliyepokea majibu kwa niaba ya mwingine kama ilivyoelezwa katika sheria hii, anawajibika kutunza siri kufuatia majibu ya VVU.

5.2 Mambo yanayoweza Kutokuzingatia Usiri wa Kitabibu

Kifungu cha 18 cha sheria hii kinaainisha vigezo vinavyoweza kufanya mtu ama taasisi kutokuzingatia usiri wa kitabibu kama ilivyoainishwa katika sehemu zilizotangulia hapo juu. Sheria inasema kuwa, usiri wa kitabibu hautakuwa umekiukwa iwapo: -

(a) Itaendana na matakwa ya taarifa pamoja na taratibu za ufuatiliaji na tathmini;

(b) Kuwataarifu watu wengine wasio katika tasnia ya afya ambao wamhusishwa moja kwa moja na watahusishwa katika matibabu na utoaji wa huduma kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI;

(c) Katika kutii amri ya mahakama katika shauri ambalo mgogoro wake umetokana na hali ya VVU ya mtuhumiwa, au;

(d) Kutoa taarifa kwa mjumbe wa familia aliyebainishwa juu ya ndugu aliyefariki.

Sehemu ya Sita

Afya na Huduma Muhimu

6.1 Huduma za Msingi za Afya kwa Watu wenye VVU na UKIMWI

Kifungu cha 19 sheria kinasema kuwa serikali, kwa kutumia rasilimali zilizopo, inawajibika kuhakikisha kuwa kila aishiye na VVU na UKIMWI, watoto walio katika mazingira magumu na yatima wanapewa huduma muhimu za afya.

ANGALIZO: Lengo la 6 la ***Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDG)*** linalohusu kupambana na VVU/UKIMWI, malaria na magonjwa mengine. MDG inaagiza kuwe na mkakati wa kufikisha matibabu ya VVU/UKIMWI kwa watu wote wanaohitaji huduma hiyo. Hata hivyo, kwa Tanzania takwimu zinaonyesha kuwa watu laki tatu (300,000) tu wameanza kutumia dawa za ARV's kati ya watu milion moja na laki nne (1,400,000) wanaokasadikiwa kuwa wanaishi na VVU/UKIMWI hadi kufikia mwaka 2008.

Mashirika ya kijamii, mashirika binafsi na mashirika ya dini yanayojihusisha na mambo ya UKIMWI, kwa kushauriana na mamlaka za serikali katika maeneo yao, yanawajibu wa kutoa huduma za kijamii zikilenga kuzuia maambukizi ya VVU na UKIMWI, kutoa misaada na huduma nyingine muhimu.

KISA MKASA - Huduma ya Madawa: Kifungu cha 19(1), S. 24(1) & (2)

Anna mtoto wa miaka 9 anatumia vidonge vya kupunguza makali ya UKIMWI (ARVs). Alipelekwa hospitalini na bibi yake. Anna amekosa awamu mbili za dawa zake za ARV na kwa sasa hajatumia kwa wiki tano. Muuguzi alipomuliza bibi yake Anna alijibu kuwa Anna ameenda kijijini kwa sababu mama yake mdogo ambaye ni mjane ni mgonjwa na hivyo Anna ameenda kumsaidia kazi. Hivyo ndiyo maana hajamleta Anna kuchukua dawa, pia na kule alipo hakuna kliniki ya kutoa dawa hizo.

Ni madhara gani atakayoyapata mtoto Anna kwa kutotumia dawa za ARV kwa ukawaida?
Kwa mujibu wa sheria ni nani anastahili lawama kutokana na ukosefu wa dawa za ARVs?

6.2 Mipango ya Kujikimu, Stadi za Kimaisha na Kupunguza Makali ya UKIMWI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 20, Wizara ya Afya, kwa kushirikiana na wizara nyingine inatakiwa kuandaa mipango na kuandaa mafunzo kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI juu ya: -

(a) Mahitaji yao ya kujikimu;

(b) Stadi za maisha;
(c) Uanzishaji wa makundi ya kusaidiana na kupeana moyo.

6.3 Kuzuia Maambukizi kwa Kumjulisha Mwenza na Kuchukua Tahadhari

Mtu yeyote atakayekuwa na ufahamu wa hali yake ya maambukizi baada ya kupima, anawajibika: -

(a) Kutoa taarifa mara moja kwa mwenza wake ama mshiriki wake kingono;
(b) Kuchukua tahadhari zote muhimu kuzuia maambukizi kwa wengine.

Mtu aliyetajwa kwenye kifungu hapo juu cha 21 cha sheria hii, anapaswa kumwarifu mwenza wake au mshirika wake kingono madhara ya maaambukizi iwapo atafanya ngono naye, isipokuwa tu iwapo mwenza huyo anafahamu hivyo.

Vilevile, mtu yeyote atakayemnyanyasa mwenza wake ama mshirika wake kingono, aidha kwa maneno, matendo ama hali fulani inayokatazwa na sheria hii, anafanya kosa na ikithibitika atatozwa faini isiyopungua shiliki laki tano na isiyozidi shilingi milioni moja au kutumikia kifungo kisichopungua muda wa miezi mitatu na kisichozidi muda wa miezi sita ama vyote viwili kwa pamoja naani faini na kifungo.

Kisa Mkasa 1 – Elimu/Uelewa (Kifungu cha 2(2), Kifungu cha 7 na kifungu cha 20

Bwana Jumanne alikuwa ameoa tokea mwaka 2007 na sasa ni miaka miwili imepita. Mke wake alilazwa hospitalini na ikabainika kuwa alikuwa ana UKIMWI. Baadaye alikufa akimwacha mume wake Jumanne mpweke. Baada ya kitambo kifupi, bwana Jumanne alianza mahusiano na mwanamke mwingine. Ila alimueleza kuwa mke wake alikufa kwa ugonjwa wa UKIMWI. Hata hivyo Bi Ashura hakuchukulia uzito suala hili. Alipata ujauzito. Baada ya siku kadhaa aliletwa hospitalini akiwa mgonjwa. Muuguzi alihisi huenda akawa na ugonjwa wa Kifua Kikuu, kichomi au UKIMWI au vyote.

Pamoja na kwamba bwana Jumanne alimweleza bi Ashura kuwa mke wake alikufa kwa UKIMWI kuna hatua yeyote ambayo angezeza kufanya ili kuzuia maambukizi kwa bi Ashura?

Kisa Mkasa 2:Wajibu wa kutoa Taarifa kwa Mwenzi – Kifungu cha 21(1) & (2)

Mzee Yusuf, baada ya kujua kuwa ni mwathirika wa ugonja wa UKIMWI, alishauriwa na muuguzi awaambie wake zake wote wawili pamoja na hawara yake. Hata hivyo, mzee Musa alimuonya kuwa endapo atafanya hivyo atapoteza hata uenyekiti wake wa kitongoji cha Mlimani. Hivyo, kwa maslahi ya chama chake, Mzee Yusufu aliamua kutowaambia wake zake na hawara juu ya hali ya afya yake. Na sasa hali imezidi kuwa mbaya.

Je, Mzee Yusuf amefanya kosa gani kulingana kwa mujibu wa sheria?
Ungekuwa muuguzi wa afya ungemshaurije mzee Yusuf?

6.4 Kuzuia na Kupambana na Magonjwa ya Zinaa

Katika harakati za kuzuia na kupambana na magonjwa ya zinaa, Kifungu cha 22 kinasema kuwa Wizara ya Afya inapaswa kuhakikisha kuwa huduma dhidi ya magonjwa ya zinaa zinaboreshwa na pia inatakiwa kuandaa mpango wa elimu kwa umma juu ya magonjwa ya zinaa na jinsi yanavyohisiana na maambukizi ya VVU na UKIMWI.

6.5 Matumizi ya Kondomu

Kondomu zinatumika kama njia mojawapo ya kupambana na maambukizo ya UKIMWI. Kuhusu hili, Kifungu cha 23 cha sheria kinatamka kuwa, Wizara ya Afya inawajibika kuhakikisha kunakuwa na kondomu za kutosha nchini kwa kuwawezesha wadau mbalimbali, kutafuta rasilimali zinazohitajika kununulia kondomu na pia kuhakikisha upatikanaji wa kondomu zenye ubora sahiki kwa viwango vya Shirika la Viwango la Taifa (TBS).

Kinyume cha masharti haya ya viwango vya ubora wa Kondomu, sheria inatamka kuwa ni kosa la jinai ambalo muhusika (mtu binafsi) anaweza kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na isiyozidi shilingi milioni thelathini au kiungo cha muda usiopungua miaka mitatu na usiozidi miaka mitano, ama adhabu zote mbili kwa pamoja yaani, faini na kifungo; na kama muhusika ni shirika au kampuni, basi litatozwa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini na isiyozidi shilingi milioni mia moja.

6.6 Kufikiwa kwa Huduma za Afya

Ufikiaji wa huduma za afya ni haki ya msingi kabisa kwa mtu yeyote. Kifungu cha 24 cha sheria hii kinatamka kuwa, mtu ambaye ni mmiliki, meneja ama mwangalizi wa huduma za afya au bima za afya, ziwe za serikali ama binafsi analazimika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI bila ubaguzi wowote kufuatana na hali zao.

Vilevile, wizara inalazimika pale ambapo rasilimali zinaruhusu kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kurefusha maisha (ARVs) pamoja na huduma nyingine za afya na madawa kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI na kwa wale walio katika hatari ya maambukizi ya VVU.

6.7 Kuzuia Maambukizi kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto

Wizara itaratibu huduma na matibabu ya wanawake wajawazito waishio na VVU, wanawake walioambukizwa VVU wakati wa kujifungua na pia kuandaa mbinu za kupunguza maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Katika jitihada hizi za kupunguza maambukizi toka kwa mama kwenda kwa mtoto mambo yafuatayo lazima yazingatiwe:-

- Watu waliofunzwa na wenye taaluma wanapaswa kutoa huduma za ushauri kwa wanawake wajawazito na wanaonyonyesha wanaoishi na VVU na UKIMWI na waume au wenza wao.
- Wanaotoa huduma za afya watafuatilia, watatoa matibabu na kutumia mbinu zote muhimu ili kupunguza maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.
- Huduma za afya inabidi zipewe kipaumbele ili kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Kisa Mkasa – Maambukizi toka kwa Mama kwenda kwa Mtoto: Kifungu cha 25

Carolina, ni mama wa umri wa miaka 26, aliyempeleka mwanae katika kliniki ya VVU. Kabla ya kuzaliwa mtoto huyo, wakati wa mahudhurio ya kawaida ya kliniki, Carolina alipimwa na kugundulika kuwa anaishi na VVU. Alipewa hudma za ushauri na jinsi ya kuweza kukinga maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Carolina alifuata maelekezo yote aliyopewa ili kumkinga mwanae dhidi ya maambukizi. Carolina aliamini kuwa mwanae atakuwa salama. Kwa bahati mbaya, wakati mtoto wake anatimiza umri wa miezi 19, Carolina anashauriwa kumpima pia mwanaye VVU. Vipimo vinaonyesha kuwa naye ameambukizwa. Carolina haamini majibu hayo, kwani alifanya kila aliloambiwa ili kukmkinga mwanaye. Carolina anachukia na kugombana na wahudumu wa afya.

Je, taarifa aliyopewa Carolina ilikuwa sahihi na ya kutosha?

6.8 Kuambukizwa Ugonjwa wa UKIMWI wakati wa Matibabu

Madaktali na wauguzi wanao wahudumia wagonjwa wa UKIMWI wako hatarini kupata maambukizi ya UKIMWI kwa sababu ya aina ya kazi zao. Kwa kutambua hili, sheria hii, kupitia Kifungu cha 26 kimetoa ulinzi wa haki zao. Kifungu hicho kinasema kuwa, mtaalamu wa afya aliye katika hatari ya kuambukizwa au aliyeambukizwa VVU na UKIMWI, atakuwa na haki ya: -

(a) Kupata huduma ya kinga ya dharura baada ya kuwa katika mazingira hatarishi;
(b) Kupata matibabu au huduma endelevu za afya pindi afanyiwapo vipimo vya VVU, na;
(c) Fidia kwa madhara ya moja kwa moja aliyoyapata kutokana na kuambukizwa VVU.

6.9 Taarifa Potofu

Habari zote na taarifa zote kuhusu tiba ya VVU na UKIMWI ni lazima ziidhinishwe na tafiti za kisayansi kabla ya kutangazwa. Kutangaza habari na taarifa hizo ni lazima ziambatanishwe na ushahidi wa kabla na baada ya majaribio hayo kufanywa. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 27 cha sheria hii ya UKIMWI.

Kifungu hicho pia kinasema kuwa, mtu yeyote atakayesababisha au atakayetoa taarifa zisizo sahahi ama taarifa kuhusu tiba, kinga ama mbinu za kupambana na VVU na UKUMWI kinyume na kifungu hiki cha sheria atakuwa ametenda kosa na atakapothibitika atatozwa faini isiyopungua shilingi milion moja ama kifungo kisichopungua miezi sita, ama adhabu zote mbili kwa pamoja.

Sehemu ya Saba

Unyanyapaa na Ubaguzi

7.1 Kuzuia utungwaji wa Sheria, Sera na Taratibu za Kiubaguzi

Kama ilivyo katika Katiba ya Tanzania, Kifungu cha 28 cha sheria ya UKIMWI kinakataza aina zote za unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na VVU na UKIMWI. Kifungu hicho kinasema kuwa, ni marufuku kwa yeyote kuandaa Sera au kutunga sheria inayobagua moja kwa moja ama kwa matokeo yake watu wanaoishi na VVU na UKIMWI, watoto yatima au hata familia zao.

ANGALIZO: ***Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977*** katika Ibara ya 13, inakataza aina yoyote ile ya ubaguzi dhidi ya mtu yeyote hata kama ni mgonjwa, mtoto, au vinginevyo. ***Sheri ya Kazi na Mahusiano Kazini ya 2004*** katika Kifungu cha 14, inakataza ubaguzi wa ajira kwa kigezo cha UKIMWI.

Ufafanuzi zaidi juu ya ubaguzi na unyanyapaa umetolewa na ***Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2001***. Katika Sura ya 4, kipengele cha 1(c) imetamkwa kwamba; "Kuambukizwa UKIMWI hakutakuwa msingi wa kubaguliwa katika elimu, ajira, afya na huduma nyingine yeyote ya kijamii. Upimaji wa VVU kabla ya kupatiwa ajira hautahitajika. Watu ambao tayari wameajiriwa hawatahitajika kupima VVU moja kwa moja au kwa namna fulani. Maambukizo pekee ya VVU hayamaanishi kwamba mtu hafai kufanya kazi au kuwa msingi wa kufukuzwa kazi. Watu wenye VVU/UKIMWI watastahili kupata mafao kutoka ustawi wa jamii sawa na wagonjwa wengine miongoni mwa wafanyakazi.

Hivyo basi Katiba, Sheria na Sera mbalimbali vinakataza kutungwa kwa sheria za kibaguzi ama zinazochochea unyanyapaa hasa kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI.

7.2 Kukatazwa kwa Wahudumu wa Afya Kunyanyapaa

Kifungu cha 29 cha sheria ya UKIMWI kinatamka kuwa, mtaalamu yeyote wa afya anayeshughulika na watu wanaoishi na VVU na UKIMWI, anapaswa kutoa huduma hizo bila ya ubaguzi wala unyanyapaa wa aina yeyote ile. Kifungu hiki kinafafanuliwa zaidi na maelezo yaliyo hapo juu kuhusu Katiba, Sheria na Sera zinazokataza unyanyapaaji.

7.3 Kukatazwa kwa Aina nyinginezo za Unyanyapaa na Ubaguzi

Mbali na aina za unyanyapaa na ubaguzi vilizotajwa katika vifungu vya awali vya sheria hii, Kifungu cha 30 cha sheria hii kinaainisha aina nyingine zaidi za aina za unyanyapaa. Kifungu hiki kinamkataza mtu yeyote kufanya haya yafuatayo: -

(a) Kutokataa usajili wa mtu, ushiriki wake katika huduma au kumtoa mtu huyo katika taasisi yeyote;
(b) Kutokataa au kumzuia mtu asisafiri ndani ama nje ya nchi;
(c) Kutokumnyima mtu haki yake ya kufanya kazi;

(d) Kutokukataa ama kumzuia mtu kuishi popote, au;
(e) Kutokukataa ama kuzuia haki za mtu mwingine za makazi kwa misingi ya uhalisia, kuhisi au kudhani hali ya VVU na UKIMWI ya mtu huyo.

Hivyo basi, kwa mujibu wa Kifungu cha 31, mtu yeyote anakatazwa kumbagua au kumnyanyapaa mtu mwingine kwa misingi halisia, kuhisi ama kudhania hali yake ya VVU na UKIMWI. Kwa kuwa, watu wote ni sawa mbele ya sheria kwa Mujibu wa Ibara ya 12 ya Katiba ya Tanzania.

[Weka katuni ya mfanyakazi aliyefukuzwa kazi baada ya kutoa taarifa kwa bosi wake juu ya maambukizo aliyopata].

7.4 Makosa yatokanayo na Unyanyapaa na Ubaguzi

Kifungu cha 32 kinatamka kuwa, mtu atayekiuka masharti ya vipengele vya sehemu hii ya sheria anafanya kosa na itakapothibitika atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili ama kutumikia kifungo kisichozidi mwaka mmoja ama adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kisa Mkasa – Unyanyapaa: Vifungu vya 28 – 32

Bwana Masumbuko wa Kata ya Mwembeni amepata misukosuko sana. Awali alikuwa aajiriwe na serikali za mitaa kama mwalimu. Lakini ilipobainika kuwa ni mwathirika wa UKIMWI, Afisa Elimi wa Wilaya alimfutia usajili. Bwana Masumbuko aliamua kwenda kuishi katika kata yake. Kwa bahati nzuri alichaguliwa kuwa mjumbe wa kamati ya maendeleo ya kata. Haukupita muda napo walimtoa kwa sababu alipinga kutungwa kwa sheria ndogo zinazosema *"mgonjwa wa UKIMWI asiwe mjumbe wa kamati yoyote ya kata".*

Hali yake baadaye ikaanza kudhoofika, alipoenda katika zahanati ya Mwembeni, nesi wa zamu alikataa hata kumwandika jina katika kitabu cha wagonjwa. Alisema *"hatuna vifaa vya kuwashika wagonjwa kama wewe".* Haijulikani hali ya bwana Masumbuko kwa sasa ikoje.

Je, kuna kosa lolote kisheria limefanywa dhidi ya bwana Masumbuko?

Sehemu ya Nane

Haki na Wajibu wa Watu Wanaoishi na VVU na UKIMWI

8.1 Haki na Wajibu wa watu wenye VVU na UKIMWI, Yatima na Wengine

Mbali na haki nyingine ambazo zimeshatajwa katika kitabu hiki ambazo pia zimo katika sheria ya UKIMWI kama vile haki ya usiri, maamuzi na nyinginezo, Kifungu cha 33 kimezitaja haki nyingine za msingi kabisa kwa mtu yeyote anayeishi na VVU na UKIMWI.

Kifungu hicho kimesema kuwa, kutokana na rasilimali zitakazokuwepo, mtu yeyote anayeishi na VVU na UKIMWI ana haki ya kupata huduma ya kiwango cha juu kwa ajili ya afya ya mwili na akili pamoja na haki ya kupata huduma ya afya kutokana na magonjwa nyemelezi.

Aidha, mtu yeyote anaeishi na VVU na UKIMWI atakuwa na wajibu wa kuwalinda watu wengine dhidi ya maambukizi na kushiriki manufaa yatokanayo na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

8.2 Upatikanaji wa Huduma Muhimu za Elimu na Afya

Serikali zote za mitaa hapa nchini zina wajibu wa kuandaa na kuratibu mipango na kuratibu mikakati madhubuti itakayowasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika kupata elimu, huduma muhimu za kiafya na mahitaji muhimu ya maisha.Hii ni kwa ajili ya Kifungu cha 34 cha sheria hii.

Kadhalika, Waziri wa Afya kwa ushirikano na Waziri wa Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa wanatakiwa kuandaa kanuni zitakazotumika ili kubaini watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Kwa mujibu wa sheria hii, watoto wanaoishi katika mazingira magumu wanajumuisha pia watoto yatima.

Kisa Mafunzo - Mipango ya UKIMWI: Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Wadau Mbalimbali. Kifungu cha 34(1) Watoto katika mazingira magumu

Katika kikao cha mwezi huu cha Baraza la Madiwani, kulikuwa na mjadala motomoto. Agenda kuu ilikuwa ni ongezeko la watoto yatima katika wilaya ya Kusini. Diwani mmoja alisema halali kwake kwa sababu wananchi wanamtaka atayarishe mkakati madhubuti wa kuelezea tatizo hili la watoto yatima ambao baadhi yao wameshakuwa ni makahaba na wengine ni wezi.

Hata hivyo, wajumbe wa baraza hilo waligawanyika wengine wakisema kuwa jukumu la kutunga sera, mikakati n.k. ni la serikali kuu. Wengine walikataa. Hivyo kikao kilivunjika bila azimio lolote na hatujui sasa hatima ya watoto hawa.

Je, viongozi wa serikali za mitaa wamepewa jukumu lolote la kulinda afya za watoto yatima katika maeneo yao?

8.3 Kukatazwa kwa Matumizi mabaya ya Misaada kwa AZISE na Taasisi za Kiserikali

Kutokana na tabia ya baadhi ya mashirika na watu binafsi kutumia vibaya pesa za hisani mahusisi kwa ajili ya miradi ya UKIMWI, serikali kwa kupitia sheria hii hususani Kifungu cha 35, imetamka kuwa vitendo hivyo kimsingi ni kosa la jinai.

Kifungu hicho kinasema kuwa, makampuni, mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya kijamii, mashirika ya kidini, taasisi za kiserikali au mashirika binafsi pamoja na watu watakaopokea misaada ya aina yeyote kwa ajili ya kudhibiti maambukizi, kufanya tafiti, kutoa matibabu, kusaidia watoto yatima pamoja na watu wanaoishi na VVU na UKIMWI wanalazimika kuhakikisha kuwa misaada au huduma hizo zinawafikia walengwa ili kutimiza lengo lililokusidiwa.

Aidha makampuni, Asasi za kiraia, mashirika ya kijamii, mashirika ya kidini, taasisi za kiserikali na mashirika binafsi ambayo yatatumia vibaya misaada yakithibitika kufanya hivyo watatiwa hatiani.

Ikiwa ni mtu binafsi adhabu itakuwa ni kifungo kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka mitano au kufilisiwa mali zenye thamani ya msaada uliopokelewa. Ikiwa ni shirika lisilo la kiserikali, shirika la kidini, shirika la kijamii, shirika binafsi au kampuni, adhabu itakuwa ni kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi million tano na kisichozidi shilingi milioni hamsini.

Kampuni, shirika lisilo la kiserikali, shirika la kidini, shirika la kijamii au shirika la mtu binafsi litakalothibitika kutumia misaada ya miradi ya UKIMWI vibaya na kupewa mojawapo ya adhabu zilizotajwa hapo juu linaweza kufutiwa usajili na Msajili wa

Makampuni, Msajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali, Msajili wa mashirika ya kijamii, Msajili wa mashirika ya kidini na Msajili wa mashirika ya watu binafsi.

Kisa Mkasa - Matumizi mabaya ya fedha za miradi ya UKIMWI: Kifungu cha 35

Shirika la UWAWAU lilipokea msaada wa fedha na gari kutoka serikali ya watu wa Marekani kupitia taasisi ya USAID. Msaada huo ulikuwa ni kwa ajili ya kuwalea watoto yatima wa wilaya ya Makete amboa wazazi wao walifariki kwa ugonjwa wa UKIMWI. Walitakiwa wanunue gari na kujenga bweni kwa fedha hizo.

Hata hivyo kwa kuwa eneo hili walilokuwepo kulikuwa na tatizo la umeme, viongozi wa UWAWAU uliamua wanunue mtambo wa umeme wa sola ili uwasaidie wafanyakazi wa UWAWAU majumbani mwao. Mwezi ujao, mfadhili atatembelea miradi waliyofadhili, hivyo kwa sasa uongozi wa UWAWAU umetayarisha taarifa za matumizi ya fedha za mradi.

Je, manunuzi ya mtambo wa umeme utahesabika kama sehemu ya lengo la mradi?

Ikiwa itathibitika siyo, ni hatua gani zitachukuliwa dhidi ya uongozi wa WAWAU?

Sehemu ya Tisa

Kuanzishwa Kwa Kamati ya Utafiti

9.1 Kamati ya Taifa ya Wanazuoni wa Utafiti wa VVU na UKIMWI

Kifungu cha 36, kinaanzisha Kamati ya Taifa ya Tafiti za VVU na UKIMWI, ambayo ina jukumu la kuhakiki mapendekezo ya kufanya tafiti pamoja na kusimamia tafiti zenyewe. Kamati hii inaundwa na wajumbe wafuatao ambao huchaguliwa na Waziri wa Afya: -

(a) Mwenyekiti;
(b) Mjumbe kutoka Mpango wa Taifa wa Kuthibiti UKIMWI;
(c) Mjumbe anayewakilisha Taasisi za Elimu ya Juu;
(d) Mjumbe anayemwakilisha Mwanasheria Mkuu;
(e) Mjumbe anayewakilisha taaisi binafsi za Tafiti za Masuala ya UKIMWI;
(f) Mjumbe kutoka taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Tiba;
(g) Mjumbe kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia;
(h) Mjumbe kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili;
(i) Mjumbe anayewakilisha National Healthy Research Forum;
(j) Mjumbe anayewakilisha Asociation of Private Healthy Facilities of Tanzania;
(k) Mjumbe anaewakilisha mashirika ya watu wanoishi na Virusi vya Ukimwi;
(l) Mjumbe toka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Taratibu za kukutana na kuendesha vikao vya kamati vimetajwa katika sheria hii sehemu ya nyongeza.

9.2 Majukumu ya Kamati

Mbali na jukumu la kuhakiki mapendekezo na nia ya kufanya tafiti, kamati hii kwa kushirikiana na Taasisi nyingine, ina majukumu ya kufuatilia namna ambayo tafiti hizi zinafanywa ili kuhakikisha kuwa watu hawadhuriki. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 40 cha sheria hii.

Hivyo basi, watafiti wote wa masuala ya UKIMWI hutakiwa kuwasilisha taarifa za tafiti zao kila baada ya miezi mitatu ama sita. Pia, wanatakiwa kuwasilisha taaarifa ya matokeo ya tafiti ikiwa ni pamoja na shughuli walizofanya na kiasi cha fedha zilivyotumika. Hitaji hili ni hasa kwa wale waliopewa fedha na Mpango wa Tafiti za VVU na UKIMWI.

Taasisi zote zinatakiwa kutunza kumbukumbu za tafiti zote zinazoendelea ama zilizokamilika na pia zitawajibika kutoa matokeo ya tafiti kwa umma. Vilevile, inahitajika kuchapisha matokeo kwa lugha ya kiswahili na katika mafumo ambao watu wenye uelemavu wanaweza kuelewa.

9.3 Maadili ya Kitaaluma

Kwa mujibu wa Vifungu vya 36, 38(1), na 41(1) vya sheria hii ya UKIMWI, utafiti wowote wa kisayansi hasa kuhusu masuala ya UKIMWI unatakiwa kuhakikiwa na kuthibitishwa na Kamati ya Taifa ya Tafiti za VVU na UKIMWI, Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Tiba (NIMR) na Wizara ya Afya kwa baadhi ya tafiti.

Ifaamike pia kuwa, kwa mujibu wa Kifungu cha 41(2)(a) na (b) cha sheria hii, ni marufuku kumfanyia mtu utafiti wa aina yeyote kama mtu huyo hajafahamishwa kuhusu utafiti huo na yeye kuridhia kwa hiari yake. Na endapo muhusika ni mtoto au mtu asiyejiweza ni lazima kupata ruhusa kupita kwa mzazi wake ama mlezi wake.

Kisa Mkasa - Utafiti wa Kisayansi: Vifungu vya 36 – 42

Daktari Henkins toka nchi za nje, alikuja moja kwa moja hadi Loliondo na kutua katika uwanja wa ndege. Bila kuchelewa alikodi gari hadi kijiji cha Mashariki. Kule alikutana na viongozi wa mila. Baada ya mazungumzo mazito ya faragha, viongozi waliwakusanya watu hamsini hivi na kuwaambia kuwa Dokta Henkins alikuwa na dawa anazofanyia majaribio na kuwa eti dawa hiyo huenda ikawa ni kinga ya UKIMWI na hivyo wanajamii hao hawatalazimika kutumia kondomu ambazo hata hivyo hawazipendi.

Mmoja kati ya vijana waliochaguliwa alikataa kuchomwa dawa za Dokta Henkins kwa sababu hana hakika kuwa mtaalamu huyu ana vibali husika toka serikali ya Tanzania. Kijana huyu anachukuliwa kwenda nyuma ya ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji baada ya muda anarudi na kukubali kuchomwa dawa za Dokta Henkins. Inawezekana kuwa alihongwa ama kutishiwa maisha.

Je, Afisa Mtendaji wa Kijiji pamoja na Dokta Henkins wanaweza kushitakiwa kwa kosa lolote kisheria?

Ikithibitika kufanya kosa kisheria watapewa adhabu gani kwa mujibu wa sheria?

Sehemu ya Kumi

Ufuatiliaji wa Tathmini

10.1 Ufuatiliaji

Si rahisi kujua mwenendo wa hali ya UKIMWI hapa nchini pasipokuwa na mfumo wa kubaini mwenendo wake. Kwa kuzingatia jambo hili, sheria hii ya UKIMWI katika Kifungu 43 imeiagiza Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa, kunakuwa na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ili kupima ukubwa na mwenendo wa maambukizi ya VVU na mambo mengine yote yanayoendana na VVU na UKIMWI. Wizara inaweza kutumia TACAIDS ama mbinu nyingine yeyote ile.

10.2 Utoaji wa Taarifa kwa Huduma za Afya

Kifungu cha 44 cha sheria kinaagiza kuwa, kila mmiliki, meneja au mwangalizi wa kituo cha afya anapaswa kuasili mbinu zilizoandaliwa na Wizara kama ilivyosemwa hapo juu ili kuhakikisha utoaji wa taarifa na usiri wa kumbukumbu zote za kitabibu na kumbukumbu zote binafsi kuhusu VVU na UKIMWI, ikijumuisha taarifa zozote zinazoweza kuaptikana kwenye takwimu mbali mbali zinalindwa.

10.3 Uchunguzi wa Magonjwa na Utoaji wa Taarifa

Vile vile, taasisi zote, hospitali, maabara, kliniki na benki za damu kwenye mikoa na wilaya zinapaswa kufanya uchunguzi na kutoa taarifa za VVU na UKIMWI Wizarani. Hata hivyo, taarifa hizo zinapaswa pia kupelekwa kwenye TACAIDS ili zijumuishwe katika mkakati wa ufuatiliaji na tathmini. Agizo hili ni kwa mujibu wa Kifungu cha 45 cha sheria hii.

Sehemu ya Kumi na Moja

Makosa na Adhabu

11.1 Makosa yanayotokana na Kukiuka Haki ya Usiri

Ikumbukwe kuwa, katika sehemu zilizopita za kitabu hiki, ilitamkwa kwamba, usiri ni moja ya haki za msingi kabisa za kila binadamu. Hivyo basi ukiukwaji wa haki hii, ni kosa. Kifungu cha 46 cha sheria hii kinasema kuwa mtaalamu yeyote wa afya ama mtu mwingine awaye yote, kama ilivyoanishwa katika sheria hii: -

(a) Atakayekiuka maadili ya usiri ya utabibu, au;

(a) atakapotoa taarifa kuhusu hali ya mtu ya VVU na UKIMWI kinyume cha sheria;

Mtu huyo atakuwa amefanya kosa na pindi itakapothibitika hivyo Mahakamani atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni moja, ama kutumikia kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja ama adhabu zote mbili kwa pamoja.

11.2 Makosa yanayotokana na kuambukiza/Kuenea kwa VVU

Kifungu cha 47 cha sheria hii kimetungwa ili kuwaadhibu watu wote wenye nia mbaya ya kuambukiza wengine ugonjwa wa UKIMWI kwa njia yoyote ile. Kifungu hicho kinasema kuwa, mtu yeyote ambaye atamwambukiza mtu mwingine VVU kwa makusudi, atakuwa amefanya kosa na itakapothibitika ataadhibiwa kifungo kisichopungua miaka mitano na kisichozidi miaka kumi.

Kisa Mkasa - Kuambukiza kwa Makusudi: Kifungu cha 47

Bwana Tozi ama "Papaa" ni tajiri sana. Ni mdhamini wa bendi zote za dansi hapa nchini. Kwa kutumia nguvu yake kifedha amekuwa akitembea na mabinti wengi sana. Imekuwa rahisi kuwapata kwa sababu Papaa huhonga hata gari kwa mtu anayemtaka. Mmoja wa marafiki zake wa zamani ametoboa siri kuwa Papa ni mwathirika wa UKIMWI tokea mwaka 1995 yaani miaka zaidi ya kumi iliyopita. Na kwamba wasichana wengi wenzi wake wa zamani "aliowapitia" wameshakufa na amekuwa akiwahonga madaktari watoe majibu ya uongo pindi mwenzi wake mpya anapoenda kupima UKIMWI ili wasimjue kuwa amewaambukiza UKIMWI. Wengi wameteketea kwa ujanja wa maksudi haya ya Papaa.

Ikithibitika kwamba ni kweli Papaa amekuwa akiambukiza VVU makusudi atachukuliwa hatua gani kisheria?

Ungekuwa mganga mkuu wa mkoa ni hatua gani ungemchukulia daktari aliyekuwa akimtibu Papaa?

11.3 Makosa yanayotokana na kukiuka Taratibu za Kiusalama kunakosababisha Kuenea kwa VVU

Kuhusu ukiukwaji wa taratibu za kiusalama, ambako kunasababisha kuenea kwa VVU, Kifungu cha 48 cha sheria hii ya UKIMWI kimetamka kuwa, mtu yeyote ambaye kwa makusudi atakiuka sheria zinazohusiana na taratibu na mipango salama ya kupunguza maambukizi ya VVU atakuwa amefanya kosa, na ikithibitika: -

- Kama ni mtu binafsi, atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi laki tano ama kutumiki akifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita; au
- Kama ni kituo cha afya kitatozwa faini isiyopungua shilingi milion tatu na isiyozidi shilingi milioni tano.

Pia kituo cha afya kitakapothibitika kufanya kosa hili kinaweza kufutwa kutoka katika orodha ya vituo vya afya.

11.4 Adhabu kwa Makosa yatokanayo na Kuzuia Utekelezaji wa Sheria Hii

Sheria inasema kuwa, itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuzuia utekelezwaji kwa jinsi yoyote wa kazi zozote kama zilivyoainishwa katika sheria hii. Mtu yeyote atakaye hukumiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki, atatozwa faini isiyopungu ashilingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tano ama kutumika kifungo kisichopungua miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 49 cha sheria hii.

11.5 Adhabu za Jumla

Kuna makosa mengi sana yaliyoainishwa katika sheria hii. Baadhi ya hayo makosa yameainishiwa adhabu zake moja kwa moja. Kwa yale makosa mengine yote ambayo adhabu zake hazijatajwa katika sehemu husika, hayo adhabu yake ni kama ambavyo Kifungu cha 50 kinavyoelekeza.

Kifungu hicho, kinasema kuwa, pindi itakapothibitika kuwa mtu yeyote amefanya kosa kinyume cha vifungu vya sheria hii, kwa kila kosa isipokuwa kwa makosa yaliyoainishwa adhabu zake, atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili ama kutumikia kifungo cha muda usiopungua miezi mitatu, au kutumikia adhabu zote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Sehemu ya Kumi na Mbili

Vifungu Anuwai (Mchanganyiko)

12.1 Malalamiko

Sheria hii katika kifungu cha 51 inaelekeza kuwa, lalamiko lolote dhidi ya ukiukwaji wa vifungu na masharti ya sheria hii, yatatakiwa kuwasilishwa katika sehemu zifuatazo tena kwa maandishi: -

a) Katibu wa Kijiji au wa Kata au wa Wilaya au wa Wilaya ya Kamati za UKIMWI kutokana na kosa lilipotokea;
b) Kituo cha polisi;
c) Mmiliki, meneja au mkuu wa kituo cha afya husika; au
d) Muajiri.

Kisa Mkasa - Malalamiko/Mashitaka: Kifungu cha 51

Baada ya kuhamasishwa kuhusu haki na wajibu kama vilivyoainishwa katika Sera na Sheria za UKIMWI za Tanzania, bibi Msomi aliamua kuanza kampeni za kutetea haki za watu waliokiukiwa haki zao akiwemo bi. Amina, Emmanuel, wake wa mzee Yusuf, wateja wa shirika la UWAWAU, bwana Masumbuko, Wamasai wa kijiji cha Mashariki Loliondo na wasichana waliokuwa ni vimada wa Papaa.

Alianza kwa kupeleka baadhi ya malalamiko tena kimaandishi kwa uongozi wa kijiji, kata, wilaya na hata kamati za UKIMWI bila mafanikio. Kwa kuwa makosa yote ni ya jinai, aliamua kupeleka malalamiko katika kituo cha poilisi cha Magabi. Polisi walisema kuwa mashtaka kuhusu UKIMWI ni ya kitabibu na hivyo hawana mamlaka nayo. Bibi Msomi anasikitika sana kwa sababu alipata kusikia kuwa kuna Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2008 inayoelekeza utaratibu huo wa kushughulikia malalamiko aliyoufuata, iweje sasa uongozi wa wilaya, kata, vijiji na polisi wakatae kushughulikia malalamiko hayo?

12.2 Kanuni

Sheria hii inamruhusu Waziri wa Afya kutunga Kanuni ama sheria ndogo kutokana na sheria hii ili kuelezea, namna ambavyo majibu ya upimaji UKIMWI yanaweza kutolewa; mkakati wa kusambaza ARVs; namna ambavyo ushauri wa kitaalamu unaweza kufanywa; utayarishaji na usambazaji wa taarifa kuhusu maambukizo, hali ya watu wanaoishi na VVU; na mambo mengineyo.

12.3 Zuio/katazo la kulazimisha (lazimisho)

Kifungu cha 53 kinakataza uingiliaji wa uhuru wa imani ya kidini hasa kuhusiana na UKIMWI. Sheria inasemakuwa, hakutakuwa na kikundi ama taasisi yeyote ya dini itakayo lazimishwa kufanya kitu kinyume na imani zao ili mradi tu kwa kufanya hivyo, taasisi hiyo haivunji masharti ya sheria yeyote ya Tanzania.

MUHTASARI WA SHERIA YA UKIMWI

Wajibu umeainishwa katika vifungu vifuatavyo:

i) Vifungu vya 7 – 12;
ii) Kifungu cha 13;
iii) Kifungu cha 14;
iv) Kifungu cha 19;
v) Kifungu cha 20;
vi) Kifungu cha 22;
vii) Kifungu cha 23;
viii) Kifungu cha 24;
ix) Kifungu cha 25;
x) Kifungu cha 27
xi) Kifungu cha 28;
xii) Vifungu vya 29 – 31.

Haki zimeainishwa katika vifungu vifuatavyo:

(a) Kifungu cha 15;
(b) Kifungu cha 16;
(c) Kifungu cha 17;
(d) Kifungu cha 18;
(e) Kifungu cha 24;
(f) Kifungu cha 26;
(g) Kifungu cha 28;
(h) Kifungu cha 29;
(i) Kifungu cha 33;
(j) Kifungu cha 34;
(k) Kifungu cha 41 (2).

Makosa yameainishwa katika vifungu vifuatavyo:

a) Kifungu cha 21 (3);
b) Kifungu cha 32;
c) Kifungu cha 35;
d) Kifungu cha 46.

Usimamiaji na uratibu wa tafiti umeainishwa katika vifungu vifuatavyo:

1. Vifungu vya 36 – 42.